

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz



TAARIFA KWA UMMA

MTWARA 3/06/2020

**KUMI NA NANE WAKAMATWA MAANDALIZI UBUNGE JIMBO LA
NDANDA WILAYA YA MASASI**

Ndugu Waandishi wa Habari,

UTANGULIZI:

Nimewaita hapa kwa lengo la kuujulisha umma juu kukamatwa kwa baadhi ya viongozi wa CCM katika Kata ya Mlingula pamoja na wanachama kwa kufanya kikao kisicho halali ili kushawishi uungwaji mkono kwa mgombea aliyetia nia kugombea Ubunge katika jimbo la Ndanda lililopo Wilayani Masasi mkoani Mtwara katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Tunataka pia umma wa watanzania pamoja na wakazi wa mkoa wa Mtwara wafahamu na kutuunga mkono kwani kwa pamoja tunaweza kutokomeza rushwa katika uchaguzi.

Ndugu Waandishi wa Habari,

TAKUKURU Wilaya ya Masasi tarehe 1/06/2020 ilipokea taarifa juu ya uwepo wa vikao viwili vilivyotarajiwa kufanyika saa 3:00 asubuhi na kingine saa 5:00 asubuhi siku hiyo kwenye nyumba za viongozi wa CCM katika Kata ya Mlingula.

Vikao hivyo vyote vilidaiwa kuwa na lengo la kushawishi uungwaji mkono kutoka kwa wajumbe watakao piga kura za maoni kuwachagua wagombea Ubunge Jimbo la Ndanda Wilaya ya masasi muda wa kupiga kura utakapofika.

Uchunguzi wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara umebaini kwamba, Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Mlingula, MARTINE YACOB CHINEMBA na Mwenyekiti wa CCM Tawi la Mlingula, HUSSEIN ATHUMANI BWANALI ni mawakala ambao wanatumiwa na mwanachama wa CCM ambaye pia ni Afisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA mkoa wa Dar-es-salaam. Afisa huyo aitwaye MUHAJI RASHIDI HAKIM MROPE ameonesha nia ya kugombea Ubunge katika Jimbo la Ndanda kwenye uchaguzi ujao.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika operesheni ya uchunguzi wa tuhuma hii, maafisa wa TAKUKURU Wilaya ya Masasi walifika eneo la tukio, Mtaa wa Tandika Kata ya Mlingula, nyumbani kwa Mwenyekiti wa CCM Tawi la Mlingula - HUSSEIN ATHUMAN BWANALI maarufu kama "DJ".

Katika nyumba hiyo maafisa wa TAKUKURU waliwakuta na kuwaweka chini ya ulinzi Mtia nia huyo na mawakala wake pamoja na wajumbe katika kikao hicho. Jumla yao wote walikuwa watu 18 na walifikishwa katika ofisi za TAKUKURU (W) Masasi kwa mahojiano zaidi.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Baada ya mahojiano watuhumiwa 16 ambao ni wanachama, wajumbe na baadhi ya viongozi wa CCM waliachiwa kwa dhamana siku hiyohiyo ya Tarehe 1/06/2020. Watuhumiwa wengine ambao ni MUHAJI RASHIDI HAKIM MROPE Afisa wa TRA mkoa wa Dar-es-salaam na MARTINE YACOB CHINEMBA, Katibu Mwenezi - CCM Kata ya Mlingula, walihifadhiwa mahabusu katika Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Masasi wakati uchunguzi wa awali ulipokua unaendelea hadi Tarehe 2/6/2020 walipoachiliwa kwa dhamana.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Madiwani, Wabunge pamoja na Rais, tunatoa wito kwa wanasiasa mkoani Mtwara kufuata sharia, kanuni na taratibu zote zinazohusu uchaguzi. TAKUKURU mkoa wa Mtwara inafuatilia kwa ukaribu sana nyendo zote za wanasiasa, hata wale wanaotangaza nia kwa siri. Tunawahakikishia kwamba hakuna mwanasiasa atakayeshinda kwa njia za Rushwa.

Tunawataka wanasiasa mkoani Mtwara kuacha kufanya kampeni kabla ya muda na wananchi kutokubali kurubuniwa kwa rushwa ili kumchagua au kutomchagua mgombea yeyote. **Hatutasita** kuchukua hatua stahiki kwa yeyote atakaye husika na vitendo vya Rushwa katika uchaguzi iwe kabla, wakati au baada ya uchaguzi.

Ndugu Waandishi wa Habari,

TAKUKURU (M) wa Mtwara inapenda kuwashukuru wananchi na wadau wote kwa ushirikiano wanaotupatia katika shughuli zetu na tunaomba tuendeleo na moyo huu wa kizalendo.

Pia napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhiti Ndugu waandishi wa habari kwa ushirikiano wenu na pia nizidi kuwaomba kutuunga mkono katika kutekeleza majukumu yetu kwa kutupatia fursa katika vyombo vyenu vya habari ili tuweze kuwaelimisha wananchi kuhusu athari na madhara ya rushwa na namna salama na rahisi ya kukabiliana nayo.

“Kataa Rushwa, Jenga Tanzania”

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

ENOCK P. NGAILO

KAMANDA WA TAKUKURU (M) MTWARA
